Mpango wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Urithi wa Kitamaduni wa Kisasa

Mpango wa Kisasa wa Kumbukumbu Zilizo Hatarini Kutoweka (MEAP) ni mpango wa ruzuku wa Maktaba ya UCLA. *Tunafadhili miradi ambayo inaweka kumbukumbu, kubadilisha kwa mfumo wa dijitali na kutoa nyezo zilizohifadhiwa zilizo hatarini ya kutoweka kutoka Karne ya 20 ya 21, ikiwemo vifaa vilivyopigwa chapa, picha, filamu, sauti, visivyodumu, na vya dijitali.*

MWITO WA MAOMBI (2022-23)

MEAP inakaribisha maombi ya miradi ya muhula wa tano ili youndwa kuhifadhi, kuweka kumbukumbu, na kuweka katika mfumo wa dijitali mikusanyiko iliyo katika hatari ya hali ya mazingira, wasiwasi wa kisiasa, vyombo vya habari visivyo endelevu, uhifadhi usiofaa, au mabadiliko ya jumla au kijamii. Ufadhili sasa unapatikana kwa Ruzuku ya Kupanga kutafiti au kuwekamikusanyiko ya nyaraka na kwa Ruzuku za Miradi kuweka kwa mfumo wa dijitali na kuchapisha mikusanyiko iliyopo.

Maombi yanafunguliwa Septemba 12, 2022
Maombi ya Awali yanatarajiwa Novemba 14, 2022
Maombi ya Kina (kwa waombaji walioalikwa) yanatarajiwa Februari 13, 2022

Maombi yote lazima yawasilishwe kupitia mfumo wa maombi wa mtandaoni wa MEAP unaopatikana meap.smapply.io. Maombi yote lazima yawasilishwe katika Kiingereza.

UFADHILI UNAOPATIKANA

MEAP inatoa ruzuku mbili katika muhula huu wa kufadhili:

RUZUKU za UPANGAJI za hadi $15,000 kwa hadi mwaka mmoja wa kazi.
Ruzuku za Upangaji zinawezatumiwa **kutathmini** au **kutafiti** mikusanyiko ya kuwekwa kwa mfumo wa dijitali au kutunzwa. Mipango itakayofanikiwa itaunda ripoti za utafiti au orodha za viwango vya vifaa ambazo zinaonyesha mikusanyiko na kuitayarisha kwa kuweka katika dijitali.

RUZUKU ZA MRADI za hadi $50,000 kwa hadi miaka miwili ya kazi.
Ruzuku za Miradi zinawezatumiwa kuweka nyaraka kwa mfumo wa dijitali au kutunza rasilimali ambazo ziko kwenye mfumo wa dijitali. Miradi inayofadhiliwa na ruzuku inafaa kuwa tayari kuanza kuweka kwenye mfumo wa dijitali ambapo ufadhili unapatikana na kutayarisha mzunguko wa maisha wa kuweka kwenye mfumo wa dijitali, ikiwemo picha, maelezo ya yaliyomo (uundaji wa metadata) na uwasilishaji wa rasilimali ya dijitali.

Vifaa vyote vya dijitali vilivyotengenezwa kupitia miradi ya MEAP vitachapishwa mtandaoni na Maktaba ya UCLA. Timu za miradi zina jukumu la kutafuta ruhusa zinazofaa kwa uchapishaji wa

wazi wakati wa kutuma ombi. Miradi ya Ruzuku za Upangaji inaweza kujenga kwa wakati bora ili kuvumbua maswali yanayohusika na haki.

USTAHIKI WA MIRADI

MEAP itatoa msaada ya kupanga, kukusanya, kubadilisha, na kuelezea nyaraka au vifaa vya kidijitali vilivyoko. Vifaa ni lazima vifikie upeo ufuatao.

- **UMRI WA KIFAA** - Kuanzia mapema katika karne ya 20 hadi sasa, ikiwezekana vifaa vingi viwe kuanzia miaka ya 1950 kurudi nyuma.
- **YALIYOMO** - Vifaa vinafaa kuweka kumbukumbu ya vipengele vya historia, jamii, utamaduni, na siasa, ikiwezekana na mkazo katika haki za jamii, haki za kibinadamu, na jumuiya zisizo na kumbukumbu.
- **MALENGO YA KIJIOGRAFIA** - Nyenzo kutoka maeneo nje ya Amerika ya Kaskazini na Ulaya zinapendelewa. Tunahimiza maombi kutoka Afrika, Visiwa vya Karibi, Amerika ya Kilatini, Mashariki ya Kati, Asia ya Kati, Kusini na Kusini-Magharibi mwa Asia na Oceania.
- **MUUNDO** - Vifaa vinaweza kuwa katika mifumo mbalimbali, ikiwemo vifaa vilivyopigwa chapa, picha, filamu, sauti, visivyodumu, na faili za dijitali (ikiwa pamoja na lakini sio tu blogu, video za simu ya rununu, kurasa za tovuti, picha za 3D, kanda za sumaku na maudhui ya mitandao ya kijamii).

Maelezo na rasilimali za ziada kwa waombaji zinapatikana kwa meap.library.ucla.edu.